**JAMHURI YA UUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA NANYUMBU**

SHULE YA SEKONDARI MKAPA

S.L.P 318

**NANYUMBU**

18.11.2025

***MAWASILIANO:***
***MKUU WA SHULE: 0654 297 094/0786 121 014***
***MAKAMU: 0784 575 283***
***MWL. MLEZI***
***MATRONI: 0683 933 994***

Mwanafunzi ……………………………………………………………………
S.L.P……………………………………………………………

**YAH: - MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MKAPA MWAKA 2026**

### *1.0 Karibu Shule ya Wasichana Mkapa.*

Kwa niaba ya kamati ya uchaguzi, ninayo furaha kukuarifu rasmi kwamba umechaguliwa kujiunga na shule hii **KIDATO CHA KWANZA** mwaka 2026. ***"ELIMU KWA UKAMILIFU"*** Maneno haya ndiyo **KAULI (MOTO)** au mwongozo wa shule yetu. Kama umeridhia kujiunga na shule hii, huna budi kuitafakari kauli hiyo na kuichukulia kwa uzito unaostahili.

Shule ya Sekondari ya Wasichana MKapa ipo umbali wa kilometa tano tu kutoka Kituo Kikuu cha mabasi cha **Mangaka** kinachoitwa **MANGAKA BUSS STAND,** Usafiri kutoka kituoni hapo kuja shuleni unapatikana.

Nauli kwa pikipiki ni shilingi **2000/=** Usafiri wa bajaji kutoka kituo cha mabasi Mangaka hadi shuleni ni kati ya shilingi **3000/=** hadi shilingi **4000/=**.Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe **05.01.2026** Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **04.01.2026.**

## *2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:-*

### *2.1* **Sare ya shule:-**

a) **Sare ya darasani**

- Sketi mbili au zaidi rangi ya bluu iliyokolea.
- Mashati mawili au zaidi meupe aina ya tomato, mikono mifupi, yenye "collar" na mfuko kwa kila shati na mikono mirefu kwa wanaovaa hijabu. **Nembo ya shati** utaipata shuleni.
- Kwa watakaovaa **hijab**, ni **Majuba** mawili ya rangi nyeupe **yanayofunika mikono**.
- Sweta moja rangi ya bluu iliyokolea (Dark blue) yenye nembo ya shule
- T-shirt mbili rangi ya kijivu zenye nembo ya shule zinapatikana Shuleni

**Sare za Shule anazokuja nazo mwanafunzi**

- Viatu vyeusi vya kufunga kwa Kamba pea mbili, vyenye visigino vifupi (muundo kama viatu vya kiume) **aje navyo**.
- Soksi nyeupe jozi mbili (02) zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi **aje nazo**.

b) **Sare za michezo:-** Raba nyeusi, track suit rangi ya bluu bahari (light blue).

c) Wanafunzi watavaa sare ya darasani **wakati wa vipindi**. Wakiwa nje watavaa T-shirt na sketi au tracksut. Nguo za nyumbani **HAZIRUHUSIWI KABISA**, hivyo **asije nazo**. **Siku ya kuripoti, mwanafunzi aje amevaa track suti ya shule (bluu bahari).**

d) Hakuna shamba dress zaidi ya sare zilizoorodheshwa hapo juu.

e) Aje na shuka mbili(2) za rangi ya pinki

Shule itatoa taarifa tarehe na siku ya matukio haya):

i. Siku za mzazi/mlezi kuja shuleni na kuweza kuonana na mwanafunzi
ii. Siku za mahafali ya kidato cha nne na sita.
iii. Siku ya kikao cha wazazi (Mkapa Parents Day)

***3.0 Orodha ya vitu ambavyo mwanafunzi anatakiwa kuleta:-***

a) Madaftari makubwa kumi na mbili(12) (Counter books quire 3) na madaftari 12 aina ya msomi kwa ajili ya mazoezi.
b) Begi la kubebea madaftari
c) Godoro la ukubwa wa inch "4" lenye kava ngumu la kutosha kitanda cha futi "2½".
d) Blanketi moja (01).
e) Nguo za ndani za kutosha (chupi (kuanzia sita na kuendelea),
"underskirts"/shimizi, sidiria nne (04)) na nguo za kulalia (night dress).
f) Vyombo vya kulia chakula (sahani ya kufunika, kikombe na kijiko).
g) Ndoo mbili (02), kubwa moja na ndogo moja, moja (01) ya kuogea/kufulia na moja (01) ya kuhifadhia maji.
h) Kanga au kitenge (jozi moja tu)
i) Chandarua cheupe kimoja (01) cha pembe nne.
j) Taulo, mswaki na dawa ya meno, sabuni na mafuta ya kupaka.
k) Koti la mvua au mwamvuli.
l) Vitabu vya ibada kwa mujibu wa dhehebu/dini yako.
m) Sanduku kwa usalama ukiwa safarini na shuleni. Inashauriwa ununue sanduku kubwa la **BATI (tranker)** la kutosha vifaa vyako vyote lenye kufuli sehemu mbili.
n) Shule ina nakala chache za vitabu kwa ajili ya masomo utakayochukua; hata hivyo kama unaweza kupata vya kwako binafsi uje navyo.
o) Leta nakala ya cheti cha kuzaliwa **NI LAZIMA AJE NAYO**.
p) Kama una **Bima ya afya** njoo nayo, kama huna mzazi au mlezi **mkatie binti yako Bima ya Afya. CHF 5,000** AU **NHIF 51,000.**
q) "Mathematical Set", Kalamu za Wino, Risasi, Rula, Kamusi/Dictionary (02), moja ya Kingereza kwa Kiswahili (English- Kiswahili) na moja ya Kingereza (English-English).
r) **Ream mbili A4 za photocopy** kwa kila mwaka.
s) Picha tatu (Passport size) akiwa amevaa shati la shule na ya mzazi au mlezi.

t) **Vifaa vya usafi anvyopaswa kuja navyo**

   i. Hard broom (fagio la brash ngumu) 01
   ii. Fagio ya chelewa yenye mti
   iii. Lita 5 ya sabuni ya maji.
   iv. Jembe lenye mpini

   **NB: Vifaa vya usafi na godoro vinapatikana jirani na shule**

## 4.0 Afya ya mwanafunzi:-

Mara upatapo barua hii mwone **Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali** iliyo karibu nawe, ili upimwe kuthibitisha kuwa una afya ya kuweza kuedelea na masomo ya sekondari. Fomu maalum imeambatanishwa na barua hii. Mara utakapofika shuleni ioneshe ikiwa imejazwa na kugongwa muhuri katika Hospitali za serikali tu. Shule haitoi chakula maalum (special diet) kwa wagonjwa.

Hata hivyo:-

**Ni marufuku kuja na chakula cha aina yoyote hapa shuleni.**

## ***5.0 Sheria za shule:-***

a) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote.

b) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wanafunzi wanzake, kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, jiko la shule n.k.

c) Yakupasa kuweka shule, eneo lako na wewe binafsi katika hali ya usafi wakati wote.

d) Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa.

e) Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani na wakati wa kujisomea.

f) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua, ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na **Mkuu wa Shule.**

g) **Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, "earphones" pamoja na redio**.

h) Mwanafunzi haruhusiwi **kupiga simu popote** bila kibali cha uongozi wa shule, ili kuepuka upelekaji wa taarifa

zisizo sahihi kwa wazazi. Mawasiliano yote yatafanywa kupitia **ofisi ya Mkuu wa Shule tu. Kwa kutumia simu ya Shule tu na si vinginevyo.**

i) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja, au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani.

j) Mwanafunzi haruhusiwi **kufanya mazungumzo** na ndugu/jamaa yake msikitini, kanisani, au hospitalini. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane na **uongozi wa shule**.

k) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika **nyumba za walimu** au **wafanyakazi wengine** bila ruhusa maalum.

l) Mafuta yenye harufu kali, perfume/spray, poda, rangi za kucha na midomo, wanja, curl, nywele za bandia, mapambo kama bangili hereni, mikufu n.k**. havitakiwi kabisa shuleni.**

Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na kucha ndefu wala kujipamba.

m) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, wimbo wa shule, wimbo wa Tanzania Tanzania Nakupenda kwa Moyo Wote na Tazama Ramani, (Kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizi)

n) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi, (Mwanafunzi mgonjwa anapaswa kupumzika katika zahanati ya shule).

o) Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na **nywele fupi wakati wote** wawapo shuleni, urefu **unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana**. Hairuhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama kiduku, kijoti, kiseven n.k.

p) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo hapa shuleni.

q) Ni marufuku **kumruhusu mgeni** kufika katika **eneo la mabwenini**.

r) Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu ambaye si mwanajumuiya wa shule hii isipokuwa **kwa kumsalimia**.

s) Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anaruhusiwa **kumwombea ruhusa mwanafunzi** kama kuna tatizo. Pia

ndiye **atakayekuja shuleni** pindi atakapohitajika kufanya hivyo.

t) Wakati wa kufunga shule wanafunzi wote wataondoka **kwa pamoja kwa usafiri utakaoratibiwa na shule**. Hakuna **ruhusa yoyote itakayotolewa mapema** kabla ya **siku rasmi ya kufunga shule**.

u) Kama mwanafunzi atapatikana na kosa la nidhamu, mzazi au mlezi ndiye atakayetakiwa kufika shuleni na si mtu mwingine yeyote kama babu, bibi, mjomba,shangazi, kaka n.k.

v) Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.
Hivyo mwanafunzi:-

   i. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
   ii. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
   iii. Ahudhurie kwenye kazi atakayopangiwa
   iv. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call), ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba, mikutano ya darasa na maabara za shule.

w) **NI LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali (pass) cha maandishi.

## ***6.0 Mwanafunzi atafukuzwa shule au kusimamishwa masomo iwapo atapatikana na kosa kati ya haya yafuatayo:-***

a. Kutukana/kutumia lugha chafu, kumpiga mwalimu au mwanafunzi mwenzake
b. Kupigana na mwanafunzi mwenzake.
c. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine.
d. Kuolewa.
e. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya uongozi wa shule na utoro wa muda mrefu (miezi 03).
f. Biashara, ulevi na kutumia dawa za kulevya.

g. Kuingia na kushiriki kwenye vilabu vya pombe na nyumba za kulala wageni au nyumba zinazouza pombe (Guest house au Bar)
h. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
i. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani.
j. Wizi.
k. Kudharau bendera ya Taifa.
l. Makosa ya jinai.
m. Kunyanyapaa wengine.
n. Kuleta **simu ya mkononi** au **kukutwa na viambatanishi vyak**e kama charger, betri, vocha, line n.k.
o. Uasherati, ubakaji, na usagaji.
p. Kutokuhudhuria vipindi darasani au kutokufanya mitihani na majaribio kwa makusudi.
q. Kukaa au kulala bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi nje.

**TANIBIHI:**
Kama unakubaliana na **haya yote** yaliyoelekezwa na **uko tayari kuyatii** na **kuyatekeleza**; tia saini katika fomu iliyoambatanishwa. Fomu hii ya kujiunga na shule inatakiwa **irudishwe ofisini** pamoja na **fomu ya kupimwa iliyojazwa na mganga** wa hospitali **ya serikali tu**.

Nakutakia safari njema.

**KARIBU SANA MKAPA SEKONDARI**

**.............**

**REHEMA J. OLONYA**

**MKUU WA SHULE**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………………………………………………………
…………

Nimesoma na kuelewa yote yaliyoelekezwa kwenye barua ya kujiunga na shule.

Ninaahidi kuwa nitajifunza kwa bidii zangu zote, nitazingatia sheria za shule kama zilivyoainishwa, nitazifuata na nitakuwa na nidhamu wakati wote kwa manufaa yangu, ya shule na ya taifa kwa jumla.

Pia endapo nitakiuka taratibu na kanuni za shule nitakuwa tayari kurudi nyumbani kumuita mzazi/mlezi wangu ………………………………………………………………………

(Jina la mzazi/mlezi) au kusimamishwa masomo.

…………………………………………
……………………………….
……………………

**Jina na sahini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

**…………………………………………** **……………**

**AHADI YA MZAZI**

Mimi………………………………………………………………………………
Mzazi/mlezi wa ………………………………… ninaahidi kushirikiana na shule wakati wote kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata maelekezo yote na kutekeleza wajibu wake kwa shule na taifa.

……………………………………………….
…………………………..

**Saini ya Mzazi / Mlezi** **Tarehe**

**…………………**

**Namba ya simu**

**………………………**

MKAPA GIRLS SEC. SCHOOL
P.O.BOX 318
**NANYUMBU.**

DATE ………………

Ref. No………………………………………

**PART A: -**

To the Medical Officer,

…………………………………………………

…………………………………………………

**REF:**

**………………………………………………………………………………**

Please examine the above-named student as to her physical and mental fitness for being a student. Each defect will hinder a girl for Secondary Schools' education.

1. a. Eye sight ………………………………………………………
   b. Hearing ………………………………………………………
   c. Limbs …………………………………………………………
   d. Speech ………………………………………………………
   e. Venereal diseases ………………………………………………
   f. Leprosy ………………………………………………………
   g. Epilepsy ………………………………………………………
2. Neurosis ………………………………………………………
3. Other serious diseases ……………………………………………
4. Pregnancy ……………………………………………………

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a **GOVERNMENT MEDICAL OFFICER**)

I have examined the above-named student and confirm that she is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

| | |
|---|---|
| a. Eye sight …………………… | f. Leprosy …………………… |
| b. Hearing …………………… | g. Epilepsy …………………… |
| c. Limbs ……………………… | h. Neurosis …………………… |
| d. Speech …………………… | i. Other serious Diseases … |
| e. Venereal diseases ………………… | j. Pregnancy ……………… |

Name: ………………………… Signature ………… Date…………..

**STATION**……………………………………………………

**DESINATION**…………………………………………

**N.B.,** I request this form to be returned to school.

**FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1.JINA LA
MWANAFUNZI……………………………………………………………………

2.JINA LA MZAZI/MLEZI WA
MWANAFUNZI……………………………………

3. KAZI YA MZAZI/ MLEZI WA
MWANAFUNZI…………………………………………

4.JINA LA SHULE
ANAKOTOKA……………………………………………………

5.TAREHE YA
KUZALIWA…………………………………………………………………

6.KATA ANAYOTOKA
MWANAFUNZI……………………………………………

7.WILAYA ANAYOTOKA
MWANAFUNZI…………………………………………

8.MKOA ANAOTOKA
MWANAFUNZI……………………………………………

9.KABILA…………………………………………………………………………
………..

10.URAIA……………………………………………………………………….
………

11.DINI/DHEHEBU……………………………………………………….
………..

12.ANUANI YA
MZAZI/MLEZI………………………………………………………

13.NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI -
NYUMBANI……………………….

OFISINI……………………………………………………
E - MAIL ADRESS……………………………………………
ANUANI YA POSTA KWA AJILI YA KUTUMA MATOKEO YA
MITIHANI: -

…………………………………………………………………

14. MAJINA MANNE YA NDUGU WA KARIBU WALIOIDHINISHWA KUCHUKUA NAFASI YA MZAZI/MLEZI ENDAPO DHARULA ITATOKEA. **Namba 1 awe mzazi/mlezi**

| Na | JINA | UHUSIANO | ANAKOISHI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 01. | | | | |
| 02. | | | | |
| 03. | | | | |
| 04. | | | | |

**KUMBUKA**
**Mzazi/mlezi acha namba ya simu inayopatikana wakati wote siku ya kuripoti mwanafunzi.**